**Ufadhili Mdogo wa Kilimo Unasababisha Utapiamlo Zimbabwe**

Na Ignatius Banda

**BULAWAYO, Zimbabwe, Des 15 2015 (IPS)** – Mavuno duni ya kila mara yamepunguza akiba ya chakula katika kaya ya Ndodana Makhalima na hali ya lishe ya familia yake. Akiwa mkulima mdogo huko Lupane, kilomita zipatazo 110 kaskazini mwa mji wa pili kwa ukubwa nchini humo, Bulawayo, Makhalima mwenye umri wa miaka 56 amejifunza kuishi na njaa.



"Hapo zamani ningeweza kula umxhanxa (mchaganyiko wa mahindi na matikiti) na inkobe (mchanganyiko wa mahindi na karanga) mwaka mzima, lakini sasa haiwezekani," Makhalima alisema.

"Ghala yangu iko tupu na familia yangu haina chakula kabisa. Nadhani watoto wa leo hawatajua aina ya chakula kinachojenga mwili ambacho tulikula siku za zamani nilipokuwa kijana," alisema, akielezea jinsi lishe ya kaya ilivyoathiriwa katika maeneo yote ya vijijini nchini Zimbabwe.

Wakulima wadogo wadogo wa kijijini wanakabiliwa na changamoto nyingi huku Mtandao wa Kutoa Tahadhari ya Njaa (FEWSNET) ukizungumza juu ya ukame mwingine katika msimu wa mwaka 2015/16, ambao unaweza kuathiri zaidi mahitaji ya lishe katika nchi ambayo Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP) linasema mamilioni ya watu wanahitaji msaada wa chakula.

Lakini ni ufadhili wa sekta hiyo, ambayo iliwahi kuwa mchangiaji mkuu wa GDP ambao umeondoa zaidi matarajio ya kupata ahueni kwa Makhalima na mamilioni ya wakulima wengine katika maeneo ya vijijini.

Zimbabwe inahitaji mamilioni ya dola kufadhili mipango ya umwagiliaji ambayo inapatikana katika nchi nzima na wakati ambapo wizara ya hali ya hewa na idara ya huduma za hali ya hewa walitangaza mpango wa kupandikiza mawingu ili kuongeza mvua mwezi Oktoba, lakini bado mpango huu haujafanyiwa kazi.

Ofisi ya hali ya hewa pia ilitangaza kuwa ingenunua ndege ya kupandikiza mawingu, lakini idara hiyo hapo awali ilikuwa na malalamiko ya kukosa pesa na hivyo kuathiri shughuli zake. Bado haijulikani ni wapi fedha za kununulia ndege zitatoka.

Hata hivyo, wataalam wanasema upandikizaji wa mawingu unaweza kufanyika kama kuna mawingu maalum ambayo yataendana na zoezi hilo.

Akitangaza Bajeti ya Taifa Nov 26, Waziri wa Fedha Patrick Chinamasa alisema kilimo kinahitaji dola bilioni 1.7, wakati fedha iliyotengwa ilikuwa dola milioni 28 kwa ajili ya kufadhili pembejeo za kilimo kwa wakulima 300,000 wa vijijini. Katika mpango huo, wakulima wadogo wadogo watapata mbegu za mahindi na nafaka nyingine ikiwa ni pamoja na mbolea.

Lakini vyama vya wakulima vinasema kuna mahitaji mengi zaidi ya pembejeo kutokana na kilimo kinachotegemea mvua kukabiliwa na ukame wa muda mrefu. ”Umuhimu wa sekta hii unajikita katika mchango wake wa mapato ya kuuza bidhaa nje yanayofikia asilimia 30, asilimia 60-70 ya ajira na karibu asilimia 19 ya mchango wake katika GDP, na hivyo kuwa chanzo kikuu cha maisha ya zaidi ya asilimia 70 ya wakazi,” Chinamasa aliliambia Bunge katika mawasilisho ya bajeti yake.

Kwa mujibu wa Chinamasa, uzalishaii wa kilimo ambao umeshuhudia kushuka kwa asilmia 51 kuanzia msimu wa mwaka 2013/14, utafufuka kwa asilimia 1.8 pamoja na tahadhari kutoka kwa wizara ya hali ya hewa kuwa mwaka 2015/16 utakuwa mwaka wa ukame. Siku baada ya kuwakilishwa kwa bajeti, Waziri Chinamasa aliuambia mkutano wa kifungua kinywa kuwa Zimbabwe ingesaini mkataba wa dola milioni 60 na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo wa Umoja wa Mataifa (IFAD) kufadhili kilimo cha umwagiliaji ambacho wizara ya kilimo inaona kama ufumbuzi wa uzalishaji wa kilimo.

Hata hivyo, wakulima wadogo wadogo, ambao wanategemea zaidi kupata msaada wa kiufundi kutoka kwa maafisa ugani, wangekabiliwa na wakati mgumu mbeleni baada ya waziri wa fedha kutangaza kuwa maafisa hawa watapunguzwa kazi kama sehemu ya mkakati wa serikali kupunguza matumizi ya mshahara. Kupunguza wafanyakazi kunakuja wakati ambapo wakulima wanatafuta maarifa mapya ya kilimo na ujuzi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Kamati ya Tathmini ya Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Zimbabwe (ZimVAC), iliyoundwa na serikali na ambayo inaweka mikakati ya lishe vijijini kutokana na ufadhili wa Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa, inasema kuwa watu milioni 1.5 au asilimia 16 ya wakazi wote wa vijijini, wanahitaji msaada wa chakula. ZimVAC inabainisha kuwa hili ni ongezeko la asilimia 163 kutoka idadi ya mwaka jana.

Mashirika ya Kimaendeleo yamehusisha lishe na uwezo wa watu wa kuwaongoza katika maisha ya kiuzalishaji na hasa lishe ikisisitizwa kwa watu wenye mahitaji maalum kama

wale wanaoishi na VVU na UKIMWI. WFP tayari inasaidia wagonjwa wenye VVU, UKIMWI na TB kupata lishe nchini kote kupitia mpango wake wa Afya na Lishe, huku kukiwa na uwezekano wa kutoa msaada kwa mamilioni ya wagonjwa wanaoishi katika maeneo ya vijijini kwa mujibu wa wizara ya afya.

Hata hivyo, kuna wasiwasi kuwa kushindwa kwa kilimo na mavuno duni ambako kumepunguza akiba ya chakula katika ngazi ya kaya kutasababisha ugumu kwa wagonjwa wa VVU na UKIMWI kupata msaada wa lishe unaohitajika zaidi — ambalo pia ni suala la msingi kwa wanaotumia madawa ya kuongeza nguvu. Wakati wa maadhimisho ya Siku ya Chakula mwezi Oktoba yaliyoongozwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na WFP, Mratibu wa Kanda ya Kusini mwa Afrika na Mwakilishi wake nchini Zimbabwe, Swaziland na Botswana, David Phiri, alikiri kuwa Umoja wa Mataifa nchini Zimbabwe "unatambua kuwa ili kufikia maendeleo ya pamoja ya kilimo na usalama wa chakula na lishe, lazima kuwepo na programu za ulinzi wa kijamii."

Ikiwa sehemu ya jitihada za kuboresha kilimo na lishe, FAO na WFP wanatoa msaada kwa wakulima wadogo wadogo ili kutumia mbinu za kilimo zenye uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ili kusaidia serikali katika jitihada zake zinazolenga katika kusisitiza kilimo cha umwagiliaji nchini kote. Hatua hizi zinaweza kuleta ahueni kubwa inayotakiwa kwa wakulima kama Makhalima, ambao kilimo ni muhimu kwa lishe na kipato.

(End/2015)